YAH: TAARIFA YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

1.0 Utangulizi

Katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Manispaa ya Dodoma imetumia miongozo mbalimbali katika kufanikisha kazi hii, Aidha utaratibu wa kuandaa mpango shirikishi wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O & OD) ulizingatiwa katika kuibua miradi inayotokana na jamii katika ngazi ya Kata na Vijiji. Miradi ambayo itatekelezwa katika ngazi ya Kata na Vijiji imetokana na vipaumbele vya jamii kwa mfumo wa O & D.

Sheria na Miongozo iliyotumika katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019 ni pamoja na:-

1. Mwongozo wa uandaaji wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya fedha na Uchumi mwezi oktoba 2017 na Amri/Agizo namba 15, 16, 17 na 19 cha kanuni za fedha za Serikali za Mitaa (The Local Authority financial memorandum) 2009,
2. Agizo namba 15,16,17 na 19 Kanuni ya fedha za Serikali za Mitaa 2009 (The Local Authority financial memorandum) vimezingatiwa katika kuandaa makisio haya
3. Agizo 16(2) ambalo linataka jumla ya makisio ya matumizi ya kawaida kulingana na Jumla ya makisio ya mapato (MATUMIZI = MAPATO) limezingatiwa.
4. Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti 2018/2019.
5. Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.
6. Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 (2016/17 – 2021/22)
7. Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015-2020)
8. Malengo endelevu ya maendeleo (SDG) n.k.
9. Hotuba ya Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania
10. Bajeti hii pia imezingatia:-
    i. ongezeko la watu kutokana na ujio wa Serikali Dodoma

ii. Ongezeko la mahitaji ya huduma za jamii kutokana na ujio wa Serikali (ongezeko la watu) na kasi ya ongezeko la maambuki ya VVU kutokana na idadi ya watu.

1.1 VIPAUMBELE KATIKA BAJETI YA 2018/2019

Vipaumbele vikuu katika bajeti ya Manispaa ya mwaka 2018/2019 ni:-

1) Kuimarisha na kuboresha miundombinu ya utoaji huduma za jamii na uchumi katika Manispaa ya Dodoma.
2) Ukamilishaji wa Miradi viporo
3) Kuweka mazingira wezeshi yatakayosababisha kuinua na kukuza uchumi wa Halmashauri na kuinua kipato cha mtu mmoja mmoja katika Manispaa ya Dodoma
4) Kupanga, kupima ardhi na kusimamia uendelezajiwa mji wa Dodoma ili kuwa na hadhi ya Makao makuu ya Nchi.

Maeneo ya vipaumbele yanayozingatiwa katika mpango na bajeti ya mwaka 2018/19 vimegawanyika katika makundi makuu mawili kutokana na vyanzo vya fedha na kwa kuzingatia mwongozo wa uandaaji wa bajeti.

1.1.1 MAENEO YA VYANZO VYA NDANI (OWNSOURCE):

Halmashauri kwa kutumia vyanzo vya mapato ya ndani ndani kwa mwaka wa fedha 2018/2019 itatekeleza maeneo yafuatayo:-

1. Kuongeza mapato ya Halmashauri kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato,kutumia mfumo wa ki-elektronki na vifaa vya kukusanyia mapato vya ki-elekroniki (POS), kukusanya takwimu sahihi ,tathmini ya mara kwa mara na kuongeza usimamizi wa karibu kwa kila chanzo.
2. Uwekezaji wa Miradi mikubwa ya kimkakati , Kiuchumi ili kupunguza utegemezi wa Manispaa kwa Serikali kuu, kutokana na :-
   i. Fedha za Serikali,
   ii. Njia ya miradi shirikishi ya PPP
   iii. Mikopo katika Mabenki

3. Kuchangia miradi ya maendeleo kwa shughuli zilizoanzishwa na zitakazoanzishwa na wananchi kama njia mojawapo ya kuunga mkono juhudi zao.
4. Kuendelea na upimaji wa maeneo mbalimbali katika Manispaa ya Dodoma na kutwaa maeneo na kulipa fidia ili ikue kwa kuzingatia mipango endelevu ya ardhi.
5. Kufungua barabara kwa kuzingatia mipango ya ardhi katika maeneo mapya ya Upimaji
6. Kutoa huduma bora ya Afya na kujenga miundombinu ya utoaji huduma za Afya (Zahanati na Vituo vya Afya) Kujenga nyumba za watumishi na kutenga fedha kwaajili ya mchakato wa ujenzi wa Hosipitali ya Wilaya.
7. Kuboresha utoaji wa elimu kwa kuimarisha miundo mbinu ya elimu,(Kama Madarasa, Maabara na Nyumba za walimu, uhamisho wa walimu (Msingi na Sekondari) na kupeleke fedha mashuleni kwaajili ya kuchangia shughuli za uendeshwaji wa shule.
8. Kujenga na kuboresha masoko, D – center na C-center na vyoo katika maeneo muhimu ya masoko, maeneo ya wazi , minada na kuboresha mnada wa Msalato.
9. Kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika Manispaa ya Dodoma na kuhamasisha wananchi kukulima mazao ya mbegu za mafuta, korosho na kuendeleza zao la zabibu ili liwe zao kuu la biashara Dodoma.
10. Kuwezesha vikundi vya wakulima kutumia zana bora za kilimo na mashine ndogo za usindikaji mazao.
11. Kutoa mikopo kwa wanawake , vijana na watu wenye ulemavu na kusaidia makundi maalum kama ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, Albino na wazee
12. Kuboresha kitengo cha LOW COST ili kuzalisha bidhaa za ujenzi kwa gharama nafuu na kusaidia/kuharakisha ukamilishaji wa miradi ya Ujenzi (Madarasa, Maabara, Vituo vya Afya Nyumba za Watumishi nk)
13. Kujenga Mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Manispaa ya Dodoma kwa:-
    i. Kulipa madeni mbalimbali ya wazabuni na watumishi.
    ii. Kutoa vitendea kazi kwa watendaji wa Kata na vijiji.
14. Kukarabati majengo na miundombinu mbalimbali ya Halmashauri ili kuboresha utoaji wa huduma.za jamii (Maji, Afya, Elimu n.k)

15. Kuendelea kuelimisha jamii kuhusu lishe bora na kupambana na udumavu wa watoto chini ya miaka mitano.
16. Kuimarisha miudombinu na kuboresha matumizi ya TEHAMA.
17. Kuimarisha huduma za uzoaji, uchambuzi, usafirishaji na uzikaji salama wa taka ngumu.
18. Ujenzi wa machinjio ya kisasa ya Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma.
19. Kupima na kutengeneza hati maeneo yanayomilikiwa na Halmashauri
20. Kujenga mitaro ya miundombinu ya barabara katika makazi mapya
21. Kujengea uwezo Mabaraza ya Kata.

Aidha katika bajeti hii ya Mwaka wa fedha 2018/2019 fedha zilizoelekezwa kwenye miradi ya Maendeleo ni shilingi 54,560,816,638.00 sawa na asilimia 81.00 ya bajeti yote ambayo ni shilingi 67,149,647,027.00 ya mapato ya ndani.

1.1.2 RUZUKU KUTOKA SERIKALI KUU NA WAFADHILI

Maeneo yaliyopewa kipaumbele kutokana ruzuku kutoka Serikali Kuu na wafadhili ni kama ifuatavyo:-

1. Kulipa mishahara ya watumishi na shughuli za uendeshaji.
2. Kuwasilisha asilimia 20 ya GPG kwa shughuliza serikali za mitaa.
3. Kukamilisha ujenzi wa maabara,vyumba vya madarasa,nyumba za watumishi katika shule za Sekondari na shule za msingi na Sekta ya Afya.
4. Kukamilisha miradi viporo iliyoanzishwa na wananchi
5. Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa maji safi na salama kupitia mradi wa Maji na usafi wa Mazingira Vijijini (RWSSP).
6. Kuboresha upatikanaji wa huduma za Afya kwa kununua madawa na vifaa tiba, ujenzi na ukarabati wa kutolea huduma za afya na nyumba za watumishi.
7. Uendeshaji wa elimu bure, mitihani na kupeleka ada mbadala (capitation), chakula fedha za madawati katika shule za msingi na sekondari.
8. Kuwajengea uwezo watumishi na Waheshimiwa Madiwani.

1.2 MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2016/17

Bajeti:

Katika mwaka wa fedha 2016/17, Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya Tshs **70,020,512,402** kama ifuatavyo:-

1. VYANZO VYA HALMASHAURI - TSHS. 3,938,132,295.00
2. MISHAHARA (PE) - TSHS 44,231,221,400.00
3. MATUMIZI MENGINEYO (OC) - TSHS. 4,815,720,524.00
4. MIRADI YA MAENDELEO - TSHS 14,035,438,183.00

JUMLA **TSHS 67,020,512,402.00**

Utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 hadi kufikia mwisho wa mwezi Juni 2017 kwa vyanzo vyote vya mapato ya ndani,ruzuku ya serikali kuu na mishahara ulikuwa kama ifuatavyo:-

1.3 MAPATO 2016/17

Jedwali Na.1: Utekelezaji wa bajeti 2016/2017 hadi Juni 2017

NA	CHANZO CHA MAPATO	BAJETI 2016/17	MAPATO HADI JUNI 2017	ASILIMIA YA MAPATO
1.	VYANZO VYA HALMASHAURI	3,938,132,295.00	4,857,698,041.00	123.3
2.	MISHAHARA (PE)	44,231,221,400.00	42,594,850,817.00	96.3
3.	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	4,815,720,524.00	1,874,437,848.00	30
4.	MIRADI YA MAENDELEO	14,035,438,183.00	11,198,136,406.00	78
	JUMLA	**67,020,512,402.00**	**60,525,123,112**	**90.0**

NB: Makisio ya bajeti ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2016/17 yalipungua kutoka **6,938,132,295.00** hadi kufikia **3,938,132,295.00** baada ya TRA kuchukua chanzo cha kodi ya majengo ambacho kilikua Tshs **3,000,000,000.00**

1.3.1 MATUMIZI

Kwa upande wa matumizi hadi kufikia mwezi Juni 2017, Halmashauri ilikuwa imetumia kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 2: Matumizi kwa bajeti ya 2016/17 hadi Juni 2017

NA	CHANZO	BAJETI 2016/2017	MATUMIZI HADI JUNI 2017	% YA MATUMIZI
1.	VYANZO VYA HALMASHAURI	3,938,132,295.00	4,580,311,419.00	116.3
2.	MISHAHARA (PE)	44,231,221,400.00	42,594,850,817.00	96.3
3.	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	4,815,720,524.00	1,874,437,848.00	39.0
4	MIRADI YA MAENDELEO	14,035,438,183.00	11,198,136,406.00	102.0
	JUMLA	**67,020,512,402.00**	**60,247,736,490.00**	**94.5**

Aidha mchanganuo wa mapato ya ndani ,OC na Miradi inaonesha katika majedwali. Kiambatisho Namba.....

1.3 .2 MAPITIO YA BAJETI YA MWAKA 2017/2018 HADI DISEMBA 2017

1.3.2.1 Bajeti

Katika mwaka wa fedha 2017/18, Halmashauri iliidhinishiwa kukusanya na kutumia jumla ya Tshs **79,523,159,820.00** kama ifuatavyo:-

1. VYANZO VYA HALMASHAURI - TSHS. 7,310,951,477.00
2. MISHAHARA (PE) - TSHS. 45,228,560,400.00
3. MATUMIZI MENGINEYO (OC) - TSHS. 3,503,800,000.00
5. MIRADI YA MAENDELEO - TSHS. 19,718,499,820.00

JUMLA **TSHS. 75,761,811,697.00**

Utekelezaji wa bajeti hiyo hadi kufikia mwisho wa mwezi Desemba 2017 ulikuwa kama ifuatavyo:-

1.3.2.2 Mapato/ Mapokezi 2017/18 Hadi Disemba 2017

Halmashauri kwa kipindi cha Julai hadi Disemba mwaka 2017 imeweza kukusanya fedha za mapato ya ndani,ruzuku kutoka serikali kuu na mishahara kama ifuatavyo;-

Jedwali Na.3 : Utekelezaji wa bajeti 2017/2018 hadi Disemba 2017

NA	CHANZO CHA MAPATO	BAJETI 2017/18	MAPATO HADI DISEMBA 2017	% YA MAPATO
1.	VYANZO VYA HALMASHAURI	7,310,951,477.00	4,179,534,610.00	57.1
2.	MISHAHARA (PE)	45,228,560,400.00	20,006,321,000.00	44.2
3.	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	3,503,800,000.00	1,655,109,593.00	47.0
4	MIRADI YA MAENDELEO	19,718,499,820.00	2,320,648,112.00	12.0
	JUMLA	**75,761,811,697**	**28,161,613,315.00**	**37.2**

NB: Makisio ya bajeti ya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha 2017/18 yalipungua kutoka **11,068,951,477.00** hadi kufikia **7,310,951,477.00** baada ya TRA kuchukua chanzo cha kodi ya mabango ambacho kilikua Tshs **3,758,000,000.00** na kufanya bajeti kubadilika kutoka Tshs. **79,579,811,697.00** na kuwa Tshs**. 75,761,811,697**

1.3.2.3 Matumizi 2017/18 Hadi Disemba 2017

Halmashauri kwa kipindi cha Julai hadi Disemba mwaka 2017 imeweza kutumia kulingana na bajeti ya mapato ya ndani,ruzuku kutoka serikali kuu na mishahara kama ifuatavyo;-

Jedwali Na.4: Utekelezaji wa bajeti 2017/2018 hadi Disemba 2017

NA	CHANZO CHA MAPATO	BAJETI 2017/18	MATUMIZI HADI DISEMBA 2017	% YA MAPATO
1.	VYANZO VYA HALMASHAURI	7,310,951,477.00	4,053,634,483.00	55.4
2.	MISHAHARA (PE)	45,228,560,400.00	20,006,321,000.00	44.2
3.	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	3,503,800,000.00	1,312,133,000.00	37.0
4	MIRADI YA MAENDELEO	19,718,499,820.00	4,135,649,413.00	20.9
	JUMLA	**75,761,811,697**	**29,507,737,896.00**	**38.9**

1.3.2.4. MADENI YA HALMASHAURI

Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma inawadai watu na taasisi mbalimbali kiasi cha shilingi **18,490,896,838.00** na ilikua inadaiwa na watu na taasisi jumla ya shilingi **9,690,389,025.00** mchanganuo wa madeni umeambatishwa Pg. Na.....

1.4. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18

Mheshimiwa Mwenyekiti,

kwa mwaka 2017/2018, Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma ,ilipanga kufanya mambo mbali mbali kupitia idara na vitengo vyake. Hadi kufikia tarehe 31/12/2017 imeweza kutekeleza na kupata mafanikio katika mambo iliyopanga kama ifuatavyo:-

1.4.1 SEKTA YA FEDHA NA BIASHARA

1) Halmashauri imeweza kukusanya jumla ya shs. **4,053,634,483.00** kwa miezi sita ambayo ni asilimia 55 ya makisio ya mwaka mzima.
2) Tumeweza kufunga hesabu za Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma kwa wakati na kuziwasilisha kwa CAG tarehe 30/9/2017 kama sheria inavyotaka.
3) Madeni ya miaka ya nyuma kwa wazabuni na watumishi jumla ya Tzs 270,153,507 zimelipwa na kuanza kurudisha imani kwa wadau wa Halmashauri.

4) Mashine za kielektroniki 69 zimeweza kununuliwa na kuongeza ufanisi katika kukusanya mapato kwa sasakuna jumla ya mashine 156.
5) Idara zote na Vitengo vyote katika Manispaa ya Dodoma vimepata mgao wa fedha za matumizi yanayotokana na mapato ya ndani kila mwezi. Hivyo kuondoa tatizo la ukosefu wa vitendea kazi na kuweza kutoa stahiki za watumishi na Waheshimiwa Madiwani.

1.4.2 SEKTA YA ELIMU (MSINGI)

1) Ufaulu wa matokeo ya kumaliza Elimu ya Msingi umeongezeka kwa asilimia 3.23 kutoka asilimia 65 (2016) hadi asilimia 68.23 (2017) ambapo wanafunzi 6,488 wamefaulu kati ya wanafunzi 9,509
2) Jumla ya wanafunzi 16,394 wameandikishwa kuanza masomo katika Shule za Msingi, sawa na asilimia 95 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 17,197
3) Wanafunzi 243 wenye mahitaji maalum wameweza kupata huduma za elimu katika shule za Msingi sita katika mazingira rafiki yenye huduma muhimu ya chakula.
4) Madeni ya nauli za likizo za walimu zimelipwa kwa walimu 189..
5) Jumla ya Vyumba 21 vya madarasa,nyumba 3 za walimu, jengo moja la utawala na matundu 47 ya vyoo yamejengwa na kukamilika kupitia mradi wa P4R
6) Idadi ya wanafunzi wanaomaliza darasa la saba bila kujua KKK imepungua kutoka watahiniwa 11 (2015), 6 (2016) hadi kufikia 0 kwa mwaka 2017
7) Kupitia program ya EQUIP yametolewa mafunzo anuwai katika mawanda tofauti ikiwa ni pamoja na :-
    i. Mafunzo kwa walimu wa hisabati na walimu wa KKK darasa la I na II
    ii. Mafunzo ya uongozi na usimaminzi kwa walimu wakuu 94, wajumbe wa Kamati za shule 1,222 na waratibu Elimu kata 33

1.4.3 SEKTA YA ELIMU (SEKONDARI)

1) A Shule 45 kati ya shule 54 zimetembelewa na maafisa wa Idara ya Elimu Sekondari na kuendesha mafunzo ya mpango wa kupambana na maambukizi ya Ukimwi na mimba za utotoni kwa kueneza kauli mbiu “Niache nisome magauni manne”.

2) Ongezeko la wanafunzi wanaofaulu na kujiunga na kidato cha kwanza unaongezeka mwaka hadi mwaka. Mwaka 2017 jumla ya wanafunzi 4,767 walijiunga na kidato cha kwanza sawa na asilimia 86.9; na mwaka 2018 jumla ya wanafunzi 5,550 wameripoti sawa na asilimia 84 ya wanafunzi waliofulu.
3) Ufaulu wa mtihani wa upimaji wa kidato cha pili 2017 ni asilimia 75.2 ukilinanisha na mwaka 2016 ambapo ilikuwa asilimia 95.0, lakini nafasi ya wilaya kitaifa imepanda kutoka nafasi ya 82 mwaka 2016 hadi ya 35 mwaka 2017. Upandaji huu wa nafasi kitaifa umetokana na ukaguzi na ufuatuiliaji wa ufundishaji wa walimu katika shule mbali mbali.
4) Mtihani wa kidato cha nne mwaka 2017 hali ya ufaulu imepanda kutoka asilimia 64.2 kwa mwaka 2016 hadi asilimia 74.05 kwa mwaka 2017, nafasi ya wilaya kitaifa nayo imepanda kutoka nafasi ya 86 kwa mwaka 2016 hadi nafasi ya 71 kwa mwaka 2017 kati ya Halmashauri 195 kitaifa.
5) Mtihani wa kidato cha sita 2017 hali ya ufaulu imepanda kutoka asilimia 93.6 mwaka 2016 hadi asilimia 95.5 mwaka 2017, kwa mitihani ya kidato cha sita ufaulu unaridhisha kwa kuwa ufaulu ni zaidi ya asilimia tisini.
6) Jumla ya Sh. 680,500,000, zimetolewa na Programme ya lipa kulingana na matokeo (Pay for Result- P4R) kwa ajili ya Ujenzi wa madarasa mabweni, maktaba, matundu ya vyoo na uchimbaji wa kisima katika shule za Sekondari Hombolo, Ihumwa, Msalato na Dodoma Sekondari.
7) Jumla ya Sh.3, 078,504,011.97 zimetolewa na mamlaka ya wizara ya Elimu (TEA) kwa ajili ya ukarabati wa shule 3 kongwe za Sekondari, Msalato, Dodoma na Bihawana.
8) Jumla ya Tshs 84,850,780 zimetolewa kwaajili ya ukamilishaji wa madarasa ,matundu ya vyoo na maabara katika shule 10 za Sekondari kutoka katika fedha za mapato ya ndani.

1.4.4 SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA

1) Mabwawa mawili yameboreshwa kwa kuongezewa kina na kutengeneza tuta katika vijiji vya Maohmamakulu na Ipala kwa kushirikiana na Mradi wa LIC.
2) Jumla ya miche 15,963 ya Korosho imegawiwa kwa wakulima 159 na taasisi 8.

3) Jumla ya mabwawa madogo 26 ya uvunaji wa maji ya mvua yametengenezwa katika Vijiji 24.

1.4.5 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI

1) Kuku 52,000 walipatiwa chanjo dhidi nya ugonjwa wa mdondo na Gumburo na mbwa 1605 dhidi ya kichaa cha mbwa katika kata zote.
2) Uendelezaji wa ujenzi wa machinjio ndogo ya Mpunguzi
3) Jumla ya ng'ombe 64,799 wamepigwa chapa. ambapo ni sawa na asilimia 75.7
4) Ng'ombe 46,594,Mbuzi/kondoo 116,000 kuku 93,615, ngurue 1,201 wamechinjwa na kukaguliwa ili kulinda afya kwa jamii.
5) Jumla ya Tshs 73,975,600.00 zimekusanywa kutoka vyanzo vya mapato vya Minada, Uvuvi na ngozi.

1.4.6 IDARA YA MAENDELEO YA JAMII NA VIJANA

1) Jumla ya vikundi 143 vimesajiliwa, Wanawake vikundi 47, vikundi 40 na vikundi mchangaanyiko 56 vya kiuchumi .
2) Idara imefanikiwa kupitisha mikopo katika Kamati ya Mikopo yenye jumla ya Shs. 69,000,000 kati ya fedha hizo jumlaya Shs. 30,000,000 ziliingizwa katika akaunti za vikundi vya vijana 28 na vikundi vya wanawake 10 vyenye thamani ya Shs. 10,000.00 na vijana yenye thamani ya Shs. 20,000,000.00.
3) Mafunzo ya ujasiriamali, Uongozi na utawala,utunzaji takwimu za biashara na utunzaji wa fedha kwa vikundi 56, yamatolewa. Vikundi 36 vya Vijana na 20 vikundi vya wanawake.
4) Kata zote 41 zimefikiwa na kuhamasishwa mambo mbali mbali yanayohusu Mikopo midogo midogo na upatikanaji wake,UKIMWI,Mfuko wa afya ya jamii (CHF), Ukatili wa Wanawake na watoto,uhakiki wa walengwa wa kaya maskini kupitia TASAF na kusimamia ugawaji wa fedha za TASAF na Usafi wa Mazingira.
5) Madawati ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ngazi ya Kata katika kata zote 41 yameundwa.

6) Msaada wa chakula cha msaada kwa watoto wanaoishi na maambukizi ya virusi vya UKIMWI 254 katika vituo vya Makole, Matumbulu, Mirembe, St Gemma na Hombolo kimenunuliwa na kusambazwa.

1.4.7 SEKTA YA MAJI VIJIJINI

1) Kukamilika kwa mradi wa maji Kijiji cha Mkonze Chididimo, Gawaye, Michese, Chigongwe, Mchemwa, Mkoyo na Chihanga imeongeza vituo vipya 128 vya kuchota maji na kuongeza watumiaji maji wapya **32,000**.

1.4.8 IDARA YA MAZINGIRA NA USAFISHAJI

Mafanikio katika kipindi cha Julai mpaka Desemba, 2017

1) Manispaa imefanikiwa kuondosha na kupeleka dampo la kisasa jumla ya Tani **27,900** katika ya tani **35,316** zilizozalishwa (79%)
2) Jumla ya vibarua **133** wa Usafi na Mazingira wameweza kulipwa posho zao za kila mwezi zenye thamani ya Tshs. **117,000,000.00** pamoja na kupatiwa vitambulisho vya CHF pamoja na wategemezi wao.
3) Jumla ya miche **34,311** yenye thamani ya Tshs. **34,311,000.00** imezalishwa na kusambazwa katika Kata mbalimbali bure toka katika Bustani za miche za Manispaa.
4) Manispaa imefanikiwa kuendesha shughuli za utupaji wa taka na uendeshaji wa dampo la Kisasa la Chidaya kwa asilimia **100** na kuwa dampo la mfano kwa Mafunzo nchini. (Ukaguzi ulifanywa na Benki ya Dunia)

1.4.9 TEHAMA

1) Uboreshaji wa miundo mbinu ya TEHAMA mfano: Mtandao kiambo (|Local Area Network) majengo ya Elimu Msingi, Afya na Kituo cha Afya Makole.
2) Makusanyo ya Halmashauri yanakusanywa kwa kutumia mfumo na vifaa vya kielekroniki (POS) hivyo kuongeza udhibiti wa makusanyo ya ndani.
3) Kuwezesha matumizi ya Mifumo ya TEHAMA (Mfano: Fedha –Epicor LGRCIS, Utawala-Lowson, TASAF), Mipango –PlanRep, FFARS, ambayo imerahisisha utekelezaji wa kazi za kila siku za Halmashauri, GMS-Mawasiliano.
4) Matumizi ya huduma ya Intaneti katika kupata na kutoa habari na mawasiliano mbalimbali.

1.4.10. KITENGO CHA UKAGUZI WA NDANI

1) Kufanya ukaguzi kulingana na mpango wa mwaka wa kitengo
2) Kupunguza hoja za ukaguzi wa nje
3) Kutoa maelekezo namna ya kupunguza hoja kwa ngazi za chini.

1.5 CHANGAMOTO ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2017/18

Mheshimiwa mwenyekiti, Bajeti ya mwaka 2017/2018 (kuishia mwezi Desemba, 2017) ilikumbana na mambo mengi ambayo hayakuwemo kwenye bajeti lakini kutokana na umuhimu wake ilibidi yafanyike.Hali hii ilisababisha utekelezaji wa bajeti yetu kwa kipindi cha Julai-Disemba, 2017 kuathirika kwa kiasi kikubwa. Mambo yaliyoathiri utekelezaji wa bajeti yetu ni kama ifuatavyo:-

1) Mahitaji makubwa ya viwanja kutokana na Serikali kuhamia Dodoma.
2) Ukosefu wa fedha za kutwaa maeneo
3) Uharibifu wa mazingira unaosababishwa na shughuli za kibinadamu
4) Upungufu wa vifaa vya kuzolea taka
5) Bei za GPSA ambazo kwa kweli ni kubwa na mara tunapoacha kutumia tunapata hoja za ukaguzi.
6) Kuvunjwa kwa stendi kuu na Jamatini na kusababisha kukosa mapato yaliyomo ndani ya bajeti yaliyotarajiwa kukusanywa kiasi cha Tshs. **308,280,000**
7) Ushiriki mdogo wa wananchi katika kuchangia miradi ya maendeleo ambayo wao wenyewe waliianzisha.
8) Bei kubwa za matengenezo ya magari zinazotolewa na TEMESA,matengenezo ya magri yasiyokidhi vigezo na kuchelewa kutengenezwa yanapopelekwa katika gereji yao.
9) Kuwepo kwa Madeni mengi ya nyuma ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida ambayo ilibidi baadhi yake yalipwe ili kuepusha Halmashauri kupata matatizo ya kisheria na pia kwa ajili ya kuendelea kupata huduma nyingine kwani baadhi ya watoa huduma walitishia kusitisha huduma zao.

10) Upungufu wa vyumba vya madarasa 783, nyumba za walimu 1,575 na matundu ya vyoo 502 katika shule za Msingi umesababisha shughuli ya ujifunzaji na ufundishaji kutofanikiwa kwa kiwango kinachohitajika
11) Upungufu wa watumishi wenye ujuzi wa kada mbali mbali katika Idara ya afya na Idara nyingine
12) Halmashauri kutokuwa na Hospital ya Wilaya
13) Uchakavu wa majengo ya Zahanati
14) Upungufu wa nyumba za watumishi Zahanati na Vituo vya afya
15) Upungufu wa magari ya kubebea wagonjwa. Kwa sasa yapo magari matatu kati ya matano yanayohitajika.
16) Urejeshwaji hafifu wa mikopo ya akina mama na vijana inayotolewa.
17) Kutoletwa kwa Ruzuku ya miradi ya maendeleo ambako kumesababisha miradi mingi iliyopangwa kushindwa kufanyika kama ilivyopangwa.
18) Upungufu wa fedha za matumizi mengineyo (OC) zinazoletwa na hasa za malipo ya nauli za likizo.
19) Kutokuletwa kwa fedha za honoraria za wawezeshaji wa programu za Elimu ya watu wazima ikiwa ni pamoja na waewzeshaji wa madarasa ya MEMKWA NA MUKEJA.
20) Kutokuwa makini kwa jumuia za uendeshaji wa miradi ya maji na hasa katika kukusanya na kutumia fedha zinazokusanywa.
21) Maombi ya mikopo kwa ajili ya vikundi ni makubwa kuliko rasilimali fedha zilizopo.

1.5 MIKAKATI YA KUTATUA CHANGAMOTO KATIKA KIPINDI KILICHOBAKI JANUARI HADI JUNI 2018

Mikakati ya utekelezaji wa miradi katika kipindi kilichobakia ni pamoja na:

1) Kuendelea kutenga fedha katika miradi iliyo katika hatua za ukamishwaji ili kupunguza miradi viporo kuongeza kasi ya ukamilishaji wa miradi ya maabara, madarasa ya shule za msingi na sekondari, vyoo na nyumba za watumishi

2) Kuhakikisha kitengo cha Low Cost Housing Unit kinafanyakazi ili kuongeza mapato na kurahisisha ujenzi wa miradi ya Manispaa
3) Kuendelea kukusanya fedha kutoka miradi ya vijana na kina mama
4) Kuomba mikopo kutoka sehemu mbalimbali ili kuharakisha kupima viwanja
5) Kudhibiti ujenzi holela
6) Kuimarisha kitengo cha utoaji wa vibali vya ujenzi.
7) Kuihamishia stendi kuu Nane nane ili kutatua changamoto ya standi iliyopo
8) Kuendelea kununua POS ili kudhibiti mapato
9) Kuunda Vikosi kazi vya kufuatilia mapato na kukusanya takwimu katika vyanzo vya mapato ya ndani
10) Kuandaa mfumo wa Kielektroniki wa kufuatilia mafaili
11) Kutumia Watendaji wa Kata na Mitaa katika kukusanya Mapato ya mchanga , ukaguzi wa nyama
12) Kuongeza kazi ya upimaji wa viwanja na ada ya upangaji wa Mji.

2.0 MPANGO NA BAJETI YA KWA MWAKA 2018/2019

Katika mwaka 2018/19, Halmashauri ya Manispa ya Dodoma inakisia kupokea na kutumia jumla ya Tshs. **128,297,662,831.62** kutoka katia vyanzo vya mapato ya ndani,ruzuku ya serikali kuu na wafadhili kwa mchanganuo ufuatao:-

MCHANGANUO WA BAJETI

1.	VYANZO VYA NDANI (OC-OWN SOURCE)	- TSHS.	12,588,830,389.00
2.	MATUMIZI MENGINEYO (OC)	- TSHS	3,355,624,000.00
3.	MISHAHARA (PE)	- TSHS	52,746,038,100.00
4.	RUZUKU MIRADI YA MAENDELEO	- TSHS.	5,532,465,655.62
5.	MIRADI YA MAENDELEO (MAPATO YA NDANI)	- TSHS	54,074,704,687.00
	JUMLA	**- TSHS.**	**128,297,662,831.62**

MUHTASARI WA MAKISIO YA RUZUKU YA MISHAHARA KWA MWAKA 2018/2019

SUB VOTE	IDARA/VITENGO	RUZUKU	MAPATO YA NDANI	JUMLA
5000	Utawala	5,837,942,100.00	215,532,000.00	6,053,474,100.00
5007	Elimu Msingi	21,841,020,000.00		21,841020.00
5033	Kilimo	871,716,000.00		871,716,000.00
5034	Mifugo	491,976,000.00		491,976,000.00
5010	Afya	5,996,952,000.00		5,996,952,000.00
5014	Ujenzi	447,672,000.00		447,672,000.00
5017	Maji	172,872,000.00		172,872,000.00
5009	Ardhi na Maliasili	-	189,628,000.00	189,628,000.00
5008	Elimu Sekondari	17,085,888,000.00		17,085,888,000.00
	JUMLA	**52,746,038,100.00**	**405,160,000.00**	**53,151,198,100.00**

Muhtasari wa Makisio ya matumizi mengineyo (OC) 2018/19

NA.	IDARA / VITENGO	RUZUKU	OWN SOURCE	JUMLA
1	UTAWALA	93,944,000	5,313,226,112	5,407,170,112
2	FEDHA & BIASHARA	3,660,000	1,694,857,129	1,698,517,129
3	ELIMU YA MSINGI	1,224,400,000	232,452,186	401,848,146
4	KILIMO	19,936,000	137,942,196	157,878,196
5	MIFUGO	16,275,000	120,707,803	136,982,803
6	AFYA	184,159,000	427,047,709	611,206,709
7	UJENZI	20,834,000	255,289,270	276,123,270
8	MAJI	10,755,000	125,321,214	136,076,214
9	UCHAGUZI	0	105,299,647	105,299,647
10	SHERIA	0	259,126,313	259,126,313
11	MIPANGO	5,490,000	913,039,425	918,529,425
12	M/JAMII	3,660,000	184,193,031	187,853,031
13	ARDHI & MALIASILI	7,320,000	1,328,909,946	1,336,229,946
14	MANUNUZI	0	256,242,524	256,242,524
15	UKAGUZI WA NDANI	5,490,000	210,694,524	216,184,524

16	ELIMU SEKONDARI	1,752,381,000	140,561,342	190,476,342
17	NYUKI	3,660,000	15,482,227	19,142,227
18	USAFI MAZINGIRA	3,660,000	438,591,768	442,251,768
19	MAWASILIANO & HABARI	0	508,493,975	508,493,975
	JUMLA	**3,355,624,000**	**12,588,830,389.00**	**15,944,454389.0**

MUHUTASARI WA BAJETI YA MIRADI YA MAENDELEO 2018 /2019

NA.	JINA LA MRADI	FEDHA ZA NDANI	FEDHA ZA NJE	JUMLA
1	RUZUKU YA MAENDELEO (CDG)	1,778,675,401	0	1,778,675,401
2	RUZUKU YA MAENDELEO (CBG)	197,630,000	0	197,630,000
3	MFUKO WA AFYA (BF)	996,520,000	0	996,520,000
4	MFUKO WA JIMBO (CDCF)	70,776,000	0	70,776,000
5	MAPATO YA NDANI	54,074,704,687	0	54,074,704,687
6	TASAF	1,703,453,363.62	0	1,703,453,363.62
7	SEDEP	335,484,000	0	335,484,000
8	EGPAF	0	448,199,800	448,199,800
9	NWSSP	449,926,891	71,600,000	521,526,891
	JUMLA	**59,607,170,342.62**	**519,799,800**	**60,126,970,142.62**

MAPITIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA MWAKA 2016/2017, 2017/2018

(JULAI 2017 – DISEMBA, 2017) NA MAKISIO YA BAJETI YA MAPATO YA NDANI YA MWAKA WA FEDHA 2018/2019.

NA.	KIANZIA	MAKISIO YA MWAKA 2016/2017	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2016 HADI JUNI , 2017	MAKISIO YA MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2017 HADI Desemba , 2018	BAJETI YA MWAKA 2018/2019
1	2	3	4	5	6	7
1.	Ushuru wa Huduma (City Service levy)	600,000,000	1,166,840,725	800,640,024	499,323,493	903,234,600
2.	Kodi ya Pango la Nyumba	215,670,000	111,994,589	96,368,000	116,814,196	696000000
3.	Maegesho ya magari	162,847,483	84,523,781	223,329,000	89,342,743	276,670,000
4.	Ada ya vyoo na maji taka	66,605,000	83,536,090	114,635,000	63,037,000	123,765,000
5.	Ada ya kupima afya	17,600,000	24,475,250	24,000,000	12,026,925	24,000,000
6.	Uchangiaji afya (Cost sharing)	0	205,945,550	140,000,000	100,014,928	221,760,000
7.	CHF	0	185,728,395	560,400,000	50,597,000	560,000,000
8.	Ada ya Leseni za Vileo	24,000,000	36,635,281	32,000,000	19,192,201	80,000,000
9.	Ada ya Leseni za Biashara	-730,531,482	835,737,520	1,125,000,000	604,347,720	1,200,000,000
10.	Ada ya Kumbi za usiku na sherehe	23,978,437.50	12,860,850	28,800,000	15,185,000	49,920,000
11	Ada ya maombi ya kibali			15,860,000	11,510,396	12,000,000

NA.	KIANZIA	MAKISIO YA MWAKA 2016/2017	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2016 HADI JUNI , 2017	MAKISIO YA MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2017 HADI Desemba , 2018	BAJETI YA MWAKA 2018/2019
	cha burudani					
12.	Kodi ya nyumba za kulala wageni	700,000,000	218,170,320	420,000,000	226,814,004	420,000,000
13.	Ushuru wa Masoko na Vizimba	230,600,000	148,813,170	311,126,000	98,069,301	829,906,000
14.	Ushuru wa Mifugo (Minada)	65,109,240	43,171,533	69,000,000	37,033,032	73,161,000
15.	Ada ya Machinjio	54,600,000	24,889,008	55,153,500	33,114,840	63,544,800
16.	Ushuru wa standi	87,152,517	187,369,340	306,000,000	90,010,787	306,000,000
17.	Ushuru wa mazao	90,500,000	107,503,467	114,227,875	36,699,000	57,940,500
18. 19.	Ushuru wa Matangazo/Mabango	550,000,000	191,395,280			
20.	Ada ya Uharibifu wa barabara	11,756,135	13,901,000			
21.	Kodi ya Ardhi (30%)	36,000,000	45,224,808	72,000,000	88,396,442	1,000,000,000
22.	Ushuru wa mazao ya misitu	72,400,000	14,645,684	48,600,000	24,411,596	48,600,000
23.	Mfuko wa Upimaji viwanja na kuuza	100,000,000	849,735,000	608,000,000	1,206,330,995	58,000,000,000
24.	Ukaguzi wa Majengo	18,440,000	17,864,186	23,000,000	11,555,000	82,332,452
25.	Mapato yanayaotokana na leseni za Pikipiki na Bajaji (50%)	5,197,400	16,512,000	8,000,000	16,661,000	19,200,000
26.	Faini kwa kuvunja sheria	41,000,000	42,703,180	44,922,098	50,186,343	315,584,196

NA.	KIANZIA	MAKISIO YA MWAKA 2016/2017	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2016 HADI JUNI , 2017	MAKISIO YA MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2017 HADI Desemba , 2018	BAJETI YA MWAKA 2018/2019
27.	Upangishwaji wa maeneo ya wazi			119,526,480	36,894,120	142,093,536

NA.	KIANZIA	MAKISIO YA MWAKA 2016/2017	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2016 HADI JUNI , 2017	MAKISIO YA MWAKA 2017/2018	JUMLA YA MAKUSANYO JULAI 2017 HADI Desemba , 2018	BAJETI YA MWAKA 2018/2019
28.	Ushuru wa madini ujenzi			252,192,000	62,406,204	300,000,000
29.	Ushuru wa namba za Bajaji na magari					23,000,000
30.	Pango la vibanda na ushuru kutoka katika D-Centre			302,100,000	30,618,890	
31.	Ushuru wa matangazo na mabango	550,000,000	191,395,280			
32.	Ada ya ukodishaji wa Mitambo			104,000,000	15,483,200	50,000,000
33.	Ada ya uzoaji taka			864,000,000	246,141,000	960,000,000
34.	Mapato mengine	58,123,038	200,382,884	456,871,500	302,499,254	
35.	Ushuru wa Samaki					1,670,500
36.	Ada ya maombi ya Viwanja					400,000,000
37.	Ada ya Ukaguzi wa viwanja					1,022,400,000
38.	Ushuru wa Ngozi					1,920,000
39.	Ushuru wa vitambulisho					6,000,000
40.	Ushuru wa kibanda cha kuuza Maji soko la Majengo					1,200,000
41.	Ushuru wa zao la nyuki					7,990,000
42.	Ada ya Minara ya Simu					222,500,000
	JUMLA KUU YA MAPATO (OWN SOURCE)	**4,512,110,733**	**5,110,642,171**	**7,469,983,477**	**4,232,271,610**	**67,149,647,027.0**

MIKAKATI YA KUKUSANYA MAPATO

1. Kuongeza vyanzo vipya vya mapato ikiwemo kuandaa na kutekeleza Miradi mikubwa ya kimkakati kwa kupata fedha kutoka 1) Serikali kuu 2) Ubia kupitia PPP na 3) mikopo kutoka katika mabenki .
2. Kuwatumia watendaji wa Kata na Mitaa ili waweze kukusanya mapato katika maeneo yao.
3. Kufanya “assessment” ya vyanzo vya mapato na kupata “data base” ili kukusanya takwimu sahaihi za vyanzo vya mapato.
4. Kuhakikisha ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo na vituo vyote unatumia mfumo wa kielectronic ili kuweza kudhibiti upotevu wa mapato.
5. Kuandaa database ya viwanja vyote vinavyozalishwa ili kudhibiti utoaji/ulipaji na uendelezaji.
6. Kuandaa mfumo wa ufuatiliaji wa mafile yote ya Halmashauri ikiwemo yanayohusu mapato.

CHANGAMOTO ZA HALMASHAURI KATIKA UTOAJI WA HUDUMA

1. Upungufu wa miundombinu ya Kutosha na yenye hadhi katika sekta ya Afya, Elimu, Maji, Barabara pamoja na nyumba za watumishi.
2. Upungufu wa Watumishi hasa katika sekta ya Afya, Elimu upande wa Sayansi, Watendaji wa Mitaa na Vijiji.
3. Mwamko mdogo wa jamii katika kuchangia shughuli za maendeleo.
4. Ukosefu wa fedha za kutosha kufanya utwaaji wa ardhi kwa ajili ya kupima viwanja kwa matumizi mbalimbali ikiwemo huduma za jamii, makazi, biashara na viwanda.
5. Uelewa hafifu wa sheria na taratibu zinazoongoza umiliki na uendelezaji wa ardhi mijini.
6. Muundo wa kiutawala uliopo hauwezeshi Halmashauri kusimamia majukumu yake kwa ufanisi katika baadhi ya maeneo ikiwemo usimamizi wa uendelezaji wa Mji.
   Upungufu wa miundombinu ya kuwezesha utoaji wa huduma za kitaifa na Kimataifa kama viwanja vya ndege, viwanja vya michezo na kumbi za mikutano